# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI



# JARIDA MAALUM LA NANE NANE 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Karibu Katika

# JARIDA MAALUM LA NANE NANE 2025

Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025.

# YALIYOMO

1. Mifugo na Uvuvi Vinara Nane Nane 2025 ..... ......................................Uk. 1
2. FETA yashika Nafasi ya Pili Nane Nane 2025......................................Uk. 4
3. TDB yang'ara Bodi ya Mazao ya Mifugo .............................................. Uk.5
4. Kishindo Paredi ya Mifugo Dodoma................................................... Uk.6
5. Tuifanye Tanzania Kuwa Kitovu cha Chakula Africa - Dkt. Mpango..... Uk.9
6. Majaliwa Aridhishwa na Sekta ya Ufugaji Samaki .............................. Uk.10
7. Matukio katika Picha Kilele cha Maonesho ya Nane Nane 2025....... Uk. 12
8. Teknolojia yatumika kudhibiti Uvuvi Haramu Bahari Kuu .................. Uk.11
9. TVLA yawagusa Wafugaji Maonesho ya Nane Nane.......................... Uk.14
10. Dkt. Mganga Akoshwa na Ndege Nyuki, Udhibiti Uvuvi Haramu......Uk. 16
11. FETA yapongezwa Mapinduzi Uchumi wa Buluu............................. Uk.17
12. TAFICO yauza Samaki wa Baharini Nane Nane Dodoma...................Uk.19
13. TDB yatoa Mafunzi ya Ubora, Usalama wa Maziwa kwa Wadau....... Uk. 21
14. Wanachama TANECU Wajifunza Tafiti za Uvuvi TAFIRI...................UK. 23
15. Bodi ya Nyama yapewa Heko Utoaji Vibali...................................... Uk. 24
16. TALIRI yaagizwa Kuibua, Kusambaza Teknolojia za Mifugo.............Uk.26
17. MPRU yabainisha Umuhimu wa Uhifadhi wa Bahari Kiuchumi........ Uk. 28
18.Matukio katika Picha za Maonesho ya Nane Nane 2025.............Uk. 30-32

# MIFUGO NA UVUVI VINARA NANE NANE 2025!

## Rais Samia aagiza Huduma za Ugani Zipatikane Mwaka Mzima Dodoma




Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bi. Agnes Meena ( Wapili Kulia) akimkabidhi Tuzo Mkurugenzi wa Maendeleo ya Miundombinu Mhandisi George Kwandu (wa Pili kushoto ) kwa niaba ya Watumishi wote mara baada ya Wizara kutunukiwa tuzo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya Mshindi wa Kwanza wa Maonesho ya Nane Nane kwa Wizara za Kisekta Agosti 8, 2025 Jijini Dodoma.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza katika kilele cha Maonesho ya Nane Nane 2025 Kitaifa Mkoani Dodoma Agosti 8, 2025 Jijini Dodoma.

Wizara hiyo imeibuka na ushindi huo baada ya kuongoza katika vigezo mbalimbali hali iliyochagizwa na maandalizi mazuri iliyofanya katika maonesho hayo huku kivutio kikubwa kikiwa ni Paredi ya Mifugo iliyoambatana na maonesho ya Ndege nyuki maalum inayotumika kwenye udhibiti wa Uvuvi haramu.

Akizungumza katika kilele cha Maonesho hayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mbali na kuipongeza Wizara hiyo kwa jitihada ilizochukua katika udhibiti wa magonjwa ya Mifugo kupitia utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo, ameielekeza kuhakikisha inaweka kituo cha Ugani kwenye viwanja vya Maonesho hayo jijini Dodoma ambavyo rasmi leo vimetambulishwa kwa jina la Dkt. John Samwel Malecela ili wananchi waendelee kunufaika na elimu ya masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya Mifugo na Uvuvi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Dkt. Ashatu Kijaji akizungumzia hali ya Sekta za Mifugo na Uvuvi wakati wa kilele cha Maonesho ya Nane Nane 2025 Kitaifa Mkoani Dodoma Agosti 8, 2025.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amemshukuru Rais Samia kwa kuiongezea Wizara yake bajeti kwa mwaka huu wa fedha ambapo amebainisha kuwa hatua hiyo imeiongeza ajira kwa watu wengi hususan wanawake na vijana. Maonesho hayo ambayo kilele chake ni Agosti 08 ya kila mwaka yataendelea kwa siku mbili zaidi kwa mwaka huu ili kuwapa fursa watu wengi zaidi kwenda kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt Ashatu Kijaji (Kushoto) akifafanua jambo Mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan ( Kulia) wakati wa Kilele cha Maonesho ya Kimataifa ya Nane Nane katika Viwanja Vya Nzuguni Jijini Dodoma, Agosti 8, 2025.

# FETA YASHIKA NAFASI YA PILI MAONESHO YA NANENANE 2025

Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) yaibuka mshindi wa pili kundi la Wakala wa Serikali wanaotoa Huduma na Uzalishaji katika Maonesho ya Kitaifa ya Nanenane yaliofanyika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.
Tuzo hiyo ilitolewa 8 Agost, 2025 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi siku ya kilele cha maonesho hayo.

Kwa mwaka 2025 FETA ilionesha teknolojia mbalimbali ambazo ni Unenepeshaji wa kaa nje ya bahari, Ufugaji wa jongoo bahari kwenye vizimba,Kilimo cha Mwani na uongezaji thamani zao la mwani.
Nyingine ni Mbinu bora za uvuvi, Kilimo na ufugaji samaki mseto, Utotoleshaji wa vifaranga vya samaki,Ufugaji wa samaki kwenye vizimba, Ufugaji wa samaki wa mapambo pamoja na utoaji wa elimu namna ya kujiunga na mafunzo yanayotolewa na wakala kupitia Kampasi zake.



# TDB YANG'AA BODI ZA MAZAO YA MIFUGO NANENANE KITAIFA 2025




Mtekinolojia wa Chakula kutoka Bodi ya Maziwa Tanzania Bw. Rajilan Hilal akionesha aina mbalimbali za vifaa vinavyotumika katika Uhakiki wa Maziwa wakati akitoa mafunzo ya Ubora na Usalama wa Maziwa ndani ya Viwanja vya Nzuguni Dodoma wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Nanenane Agosti 07, 2025

Bodi ya Maziwa Tanzania imeongoza na kupata tuzo ya Mshindi wa kwanza katika kundi la Bodi za Mazao ya Mifugo wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma

Tuzo hiyo iliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Agosti 8, 2025 wakati akihitimisha Maonesho ya Kimataifa ya Nanenane kwa mwaka 2025 itaongeza hari ya mabadiliko katika Tasnia ya Maziwa nchini.

Akiongea baada ya kupata tuzo hiyo Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania Prof George Msalya ametoa Rai wa Wadau wa Maziwa nchini kuendelea kufuata Sheria na Kanuni zinazotakiwa ili Tasnia ya Maziwa nchini iendelee Kuchangia katika pato la Taifa.


Pia ametumia Fursa hiyo kuwapongeza Watumishi wote Kwa ushirikiano wakati wote wa maandalizi wa Maonesho haya kwani ubunifu na juhudi walizozionesha wakati wa kutoa elimu na huduma kwa wananchi waliokuwa wanatembelea banda la TDB zimepelekea kupata tuzo hiyo

Mtekinolojia wa Chakula kutoka Bodi ya Maziwa Tanzania Bw. Rajilan Hilal kwa niaba ya Watumishi ameishukuru Serikali kwakuona TDB kuwa inastahili kupata Tuzo hii kwani inaonesha kuwa Taasisi inatimiza jukumu lake la Msingi katika kuwahudumia Wadau wa Tasnia ya Maziwa nchini.

Maonesho ya Kimataifa ya Nane Nane kwa mwaka 2025 yamefanyika siku kumi kuanzia Agosti 1 hadi 10, 2025 katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma kuanzia kwa lengo kutoa fursa zaidi kwa watanzania kuonesha huduma na bidhaa mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

# KISHINDO! PAREDI YA MIFUGO DODOMA

- Mifugo yenye thamani ya takribani Mil. 50.5 yashindanishwa
- Yupo Mbuzi anayezalisha lita 24 za maziwa kwa siku



Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendesha paredi maalum ya Mifugo kwenye Maonesho ya kimataifa ya Nane Nane 2025 kwa lengo la kuwahamasisha wafugaji kuachana na ufugaji wa asili na kugeukia ufugaji wa kibiashara.

Akizungumza mara baada ya kushuhudia paredi hiyo Mgeni rasmi wa tukio hilo ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule ameipongeza Wizara hiyo kwa kufanya tukio hilo kuwa na hadhi ya kimataifa ambapo jumla ya Mifugo 27 ilishindanishwa.



"Lakini pia nimeona wafugaji wameanza kubadilika kwenye suala la malisho ya mifugo yao na sasa niwaelekeze Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili mabwawa yaliyopo kwenye maeneo yenu badala ya kukaa bila matumizi yoyote yaelekezwe kwenye shughuli za Mifugo na Uvuvi" Amesema Mhe. Senyamule.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Edwin Mhede amesema kuwa mabadiliko makubwa ya Paredi ya mwaka huu ni ishara ya kukua kwa sekta ya Mifugo na Uvuvi ambapo amewataka wafugaji kutumia mafunzo waliyopata kwenye tukio hilo kama darasa la kubadili mfumo wao wa ufugaji kwenye maeneo yao.

"Sekta zetu zimeendelea kuwekeza kwenye teknolojia kama tulivyoona hivyo wito wa wizara ni kuwasihi wadau mbalimbali wa sekta hizi kuchangamkia fursa za teknolojia hizi ili mwakani mje na matokeo yanayotokana na teknolojia hizi" Ameongeza Dkt. Mhede.

Aidha Dkt. Mhede amesema kuwa Paredi hiyo mbali na kuhamasisha ufugaji wa kibiashara inalenga kuinua hali ya lishe kwa wananchi kupitia ulaji wa mazao ya Mifugo na Uvuvi ikiwa ni pamoja na nyama, samaki, maziwa na mayai.

Paredi iliyofanyika mwaka huu ni ya 15 tangu kuasisiwa kwake na Rais wa awamu ya nne Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete kwenye kilele cha Maonesho ya Nane Nane mwaka 2010.

# TUIFANYE TANZANIA KUWA KITOVU CHA CHAKULA AFRIKA-DKT. MPANGO



Makamu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpnago (Kushoto) akikagua Mifugo kwenye Mabanda ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakati wa Ufunguzi wa Maonesho ya Nane Nane 2025 Nzuguni Jijini Dodoma agosti 1, 2025.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amewataka viongozi wa sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi nchini kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha chakula katika ukanda wa Afrika.

Mhe. Dkt. Mpango amesema hayo wakati wa hotuba yake ya Ufunguzi wa Maonesho ya kimataifa ya Nane Nane aliyoitoa Agosti 1, 2025 kwenye Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma ambapo amesisitiza Viongozi hao kuwa kinara kwenye utekelezaji wa dira ya Taifa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025-2050.

“Pamoja na mambo mengine Viongozi tuna wajibu wa kuwaelekeza wakulima, wafugaji na wavuvi wetu kuweka nguvu zaidi kwenye mazao yenye thamani kubwa sokoni” Amesema Mhe. Dkt. Mpango.

Aidha Dkt. Mpango amewataka wafugaji kuwekeza katika uzalishaji wa kisasa wa bidhaa zinazotokana na mifugo ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje, kuendeleza uvuvi na ufugaji wa samaki na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye miundombinu baridi ya uhifadhi na usafirishaji wa mazao wa Mifugo na Uvuvi.

Akitoa taarifa ya Maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi nchini, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bi. Agness Meena amesema kuwa katika Maonesho ya hayo ya mwaka huu Wizara yake imejikita katika kuonesha teknolojia za kisasa kwenye uzalishaji wa malisho, ufugaji wa samaki, uzalishaji wa mazao ya Mifugo na uchakataji wa mazao ya Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kuongeza thamani, kupunguza upotevu na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

“Agosti 5 mwaka huu itakuwa ni siku ya Mifugo na Uvuvi katika Maonesho haya ambapo kutakuwa na gwaride la Mifugo na onesho la usimamizi wa rasilimali za Uvuvi kwa kutumia Ndege nyuki lakini pia inaendelea kutoa huduma ya uchanjaji na utambuzi wa Mifugo hapa hapa viwanjani” Ameongeza Bi. Meena.

Mbali na Paredi ya Mifugo kwenye Maonesho ya Nane Nane mwaka huu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliandaa Kijiji cha Protini kilichokuwa ndani Viwanjani vya Nane Nane Nzuguni Jijini Dodoma kwa lengo la kuhamasisha lishe bora itokanayo na mazao ya Mifugo na Uvuvi.



# MAJALIWA ARIDHISHWA NA MAENDELEO SEKTA YA UFUGAJI SAMAKI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameridhishwa na maendeleo ya Sekta ya Ufugaji wa samaki nchini ambapo amewataka wananchi kuelekeza nguvu kwenye tasnia hiyo ili kuongeza kiwango cha uzalishaji wa samaki nchini.

Mhe. Majaliwa ameyasema hayo Agosti 03, 2025 mara baada ya kufika kwenye eneo la mabwawa ya ufugaji samaki na vizimba lililopo kwenye banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiwa ni sehemu ya Maonesho ya kimataifa ya Nane Nane yanayoendelea kwenye viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

“Mhe. Rais amesambaza vizimba vingi vya kutosha kanda ya ziwa, nilitaka kufahamu kama tumefanikiwa” amesema Mhe. Majaliwa.

Aidha Mhe. Majaliwa ameridhishwa na gharama ya vizimba hivyo ambayo amekiri hata watu wa kipato cha chini wanaweza kuimudu huku pia akitoa rai kwa wananchi wote hususani wadau wa Uvuvi kutumia zana zilizoidhinishwa na Serikali wakati wote wa utekelezaji wa shughuli zao za Uvuvi.

Akizungumza kwa niaba ya wanufaika wenzake wa mkopo wa masharti nafuu wa vizimba hivyo Makamu mwenyekiti kutoka kikundi cha Vijana Kazini kutoka mkoani Mwanza Bw. Elisha Gayo ameishukuru Serikali kwa mkopo wa shilingi milioni 117 waliopatiwa ambapo amekiri umesaidia kubadili maisha yao kwa kiasi kikubwa.





Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassimu Majaliwa (Katikati) akitoa Maelekezo kwa Viongozi na Wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi juu ya kuendeleza Ufugaji wa Samaki kwenye Vizimba wakati wa Maonesho ya Nane Nane Agosti 4, 2025



Mkuu wa idara ya ukuzaji viumbe kwenye maji FETA Bw, Mashaka Kapagalla (kulia) akimwelezea Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ( Wakwanza, Kushoto) juu ya teknolojia mbalimbali zinazooneshwa na FETA kwenye maonesho ya Kitaifa ya nanenane jijini Dodoma Agosti 4, 2025.


UFUNGUZI WA MAONESHO YA WAKULIMA
NANENANE KITAIFA NA KIMATAIFA 2025
MAADHIMISHO YA SIKU YA
NANENANE 2025






JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
PAREDI YA MIFUGO 2025







# TVLA YAGUSA MIOYO YA WAFUGAJI MAONESHO YA NANENANE




Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imeendelea kugusa mioyo ya Wafugaji kwa kutoa huduma na elimu inayolenga kuboresha afya ya mifugo nchini.

Elimu hiyo imetolewa wakati wa maonesho ya Nane Nane 2025 yalianza Agosti 1 hadi 8, 2025 katika Uwanja wa Nzuguni, Mkoani Dodoma ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa Mgeni rasmi siku ya Kilele Agosti 8, Mwaka huu.

Akizungumza Agosti 07, 2025 katika banda la TVLA, Meneja wa Kituo cha TVLA Dodoma, Dkt. Japhet Nkangaga, amesema wakala inajihusisha na utoaji wa huduma za uchunguzi wa magonjwa ya mifugo, upimaji wa sampuli, utengenezaji wa chanjo, pamoja na tafiti za kisayansi zinazolenga kuboresha afya na uzalishaji wa mifugo nchini.

"Katika Maonesho haya ya Nane Nane mwaka huu kwa nchi zima tumetoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa kabla ya matibabu, umuhimu wa kuchanja mifugo, na madhara ya kutumia dawa bila vipimo na hadi kufikia agosti 7, kwa mkoa Dodoma pekee tumehudumia zaidi ya wadau wa mifugo zaidi ya 800." alieleza Dkt. Nkangaga.

Aidha Dkt. Nkangaga ametoa wito kwa wafugaji wote nchini kuwatumia wataalamu wa mifugo na vituo vya uchunguzi ikiwemo wataalam kutoka TVLA kwa ajili ya vipimo sahihi vinavyopatikana katika maabara ili kuchunguza na kutambua magonjwa yanayowapata wanyama, kutumia chanjo kukinga wanyama dhidi ya magonjwa na kupata ushauri wa kitaalamu.

Kwa upande wake mfugaji kutoka Wilaya ya Chamwino jijini Dodoma Bi. Gaudensia Simwanza, alisema kupitia TVLA amejifunza mambo mapya kuhusu njia sahihi za kutibu mifugo yake kwani kabla hajapata elimu alikuwa anatibu mifugo yake kwa mazoea na mara nyingi bila vipimo.
Naye Bw. Frank Mvungi, mfugaji kutoka Kongwa, alisema elimu aliyoipata kuhusu chanjo kwa mifugo ambayo inaonekana haina dalili za ugonjwa itamsaidia kanuni na taratibu bora za uchanjaji wa mifugo ili kuikinga na magonjwa.



# DKT. MGANGA AKOSHWA NA NDEGE NYUKI, KUDHIBITI UVUVI HARAMU




Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dkt. Fatma Mganga ( Wa Kwanza Kulia ) akisikiliza Maelezo juu ya ndege nyuki ya kudhibiti Uvuvi Haramu Ziwani na Baharini 'Drone ' kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Udhibiti Ubora kiutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Christian Nzowa (wakati wa Maonesho ya Nane Nane Mwaka 2025, Jijini Dodoma.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dkt. Fatma Mganga amefurahishwa na teknolojia ya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi inayotumiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye ukanda wa Ziwa Victoria.

Dkt. Mganga amebainisha hayo mara baada ya kufika kwenye banda la Wizara hiyo Agosti 02,2025 lililopo kwenye Maonesho ya kimataifa ya Nane Nane Nzuguni jijini Dodoma ambapo ameipongeza Serikali kwa kubuni mbinu hiyo ya kisasa ya ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi nchini.

“Kupitia teknolojia hii wavuvi haramu wanaweza kubainika kwa haraka na wepesi bila kutumia nguvu kubwa na kunakuwa na ushahidi tofauti na hapo awali ambapo watu wengi walikuwa wanakana kwa sababu hakukuwa na ushahidi” Amesema Dkt. Mganga.

Aidha Dkt. Mganga ameongeza kuwa uwepo wa teknolojia hiyo umesababisha kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu nchini jambo ambalo amesema kuwa litasaidia kuongeza kiwango cha samaki kwenye vyanzo vya asili.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Udhibiti Ubora Dkt. Christian Nzowa amesema kuwa Ndege nyuki hiyo ina uwezo wa kutembea hadi umbali wa kilomita 4 huku ikirekodi matukio yote yanayoendelea ziwani huku pia ikiwa na uwezo wa kubaini hatari yoyote inayojitokeza ziwani na kutuma ishara kwenye kituo cha uangalizi

# FETA YAPONGEZWA MAPINDUZI YA UCHUMI WA BULUU

Balozi Mteule wa Tanzania nchini Italia na Mwakilishi wa kudumu kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (FAO,WFP na IFAD) Bw, Mbarook Nassor Mbarouk ameipongeza Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kwa dhamira yake kubwa ya kufanya mapinduzi katika sekta ya uchumi wa buluu hususan mafunzo ya kilimo cha mwani na uongezaji thamani zao la mwani.

Balozi Mbarouk alitoa pongezi hizo Agosti 7, 2025 alipotembelea banda la FETA katika maonesho ya Kitaifa ya Nane Nane yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

"Nimefurahi kuona mmetuletea bidhaa za mwani na mnatoa mafunzo juu ya uongezaji thamani zao la mwani, hii itasaidia wananchi wengi zaidi kupata elimu na kujikwamua kiuchumi kupitia uchumi wa buluu" Amesema Balozi Mbarouk.




Balozi wa Tanzania nchini Italia Bw, Mbarook Nassor Mbarouk (Kulia) Akitoa Maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi FETA Dkt. Semvua Mzighan (Kushoto) Wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Nane Nane Mwaka 2025 Nzuguni Jijini Dodoma.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) Dkt. Semvua Mzighani amesema wakala hiyo inatoa mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu juu ya kilimo cha zao la mwani na uongezaji thamani zao la mwani hivyo ametoa wito kwa wananchi kutembelea banda la FETA kupata utaratibu wa kupata mafunzo hayo ili kuongeza kipato chao na pato la Taifa kwa ujumla.

Aidha Dkt. Mzighani ametaja teknolojia mbalimbali ambazo FETA inaonesha katika maonesho ya Nane Nane 2025 kuwa ni pamoja na Unenepeshaji wa kaa nje ya bahari, Ufugaji wa jongoo bahari kwenye vizimba, Kilimo cha Mwani na uongezaji thamani zao la mwani.

Teknolojia nyingine ni Mbinu bora za uvuvi, Kilimo na ufugaji samaki mseto, Utotoleshaji wa vifaranga vya samaki,Ufugaji wa samaki kwenye vizimba, Ufugaji wa samaki wa mapambo pamoja na utoaji wa elimu namna ya kujiunga na mafunzo yanayotolewa na wakala kupitia Kampasi zake.



# TAFICO YAUZA SAMAKI WA BAHARINI MAONESHO YA NANENANE DODOMA

Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) limefanya Biashra ya Kuuza Samaki wanapatikana Baharini Pekee katika Maonesho ya Nane Nane 2025 yaliyofanyika Kitaifa Jijini Dodoma kuanzia Agosti Mosi hadi Agosti 10, 2025 kwa lengon la kutoa fursa ya wadau kupata Protini ya Samaki wa Baharini.

Katika maonesho hayo, TAFICO Ililijikita katika kufanya biashara ya samaki na kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana pamoja na miradi iliyokamilika, inayoendelea kutekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa, na pia manufaa ya miradi hiyo kwa sekta ya uvuvi na wananchi kwa ujumla.



Samaki waliokuwa wanapatika kipindi cha Maonesho Jijini Dodoma ni Samaki wa maji chumvi (baharini) aina ya jodari (tuna), changu, kibua, barakuda, nguru (kingfish), songoro, red snapper na kolekole.

Mbali na miradi mingine, TAFICO inaendelea na ujenzi wa Meli ya Uvuvi kupitia Mradi wa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii chini ya Serikali ya Japani (ESDP Japan) ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 85.
Ujenzi wa Meli hii ni hatua muhimu kwa shirika kufanya uvuvi wa bahari kuu, mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa meli hiyo ifikapo mwezi Disemba 2025, hivyo kufanya upatikanaji wa uhakika wa samaki kwenye masoko ya ndani na kufungua fursa za masoko ya nje.

Aidha, shirika linalenga kuongeza na kuboresha mnyororo wa thamani kwenye mazao ya uvuvi kwa kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi Wilayani Kilwa ambapo upembuzi yakinifu umekwishafanyika, Pia upatikanaji wa Chakula bora cha Samaki utaimarika kwa Ujenzi kiwanda cha kuzalisha chakula cha samaki wafugwao kitakachojengwa Mkoani Mwanza.



# TDB YATOA MAFUNZO YA UBORA, USALAMA WA MAZIWA KWA WADAU

Bodi ya Maziwa Tanzania kwa kushirikiana na wadau wake imeendesha mafunzo Maalumu ya Uhakiki wa Ubora na Usindikaji wa Maziwa kwa wasindikaji wadogo na wafugaji waliotembelea banda la Bodi ya Maziwa wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni, Dodoma.

Mtekinolojia wa chakula kutoka Bodi ya Maziwa Tanzania, Rajilan Hillal amesema Bodi hiyo imetumia fursa ya Maonyesho ya Nane Nane Kitaifa kutoa mafunzo kuhusu ubora na usalama wa maziwa kwa wadau mbalimbali wa sekta hiyo.

Hillal amesema mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha wadau kutambua maziwa salama, yasiyoharibika na yaliyo bora kwa afya ya mlaji, ili waweze kuzalisha na kusindika kitaalamu.

“Tunawafundisha pia namna ya kusindika mazao makubwa mawili yanayotumika zaidi nchini, ambayo ni mtindi wa kawaida na mtindi ulioboreshwa. Lengo letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maziwa yaliyo salama na yaliyosindikwa kitaalamu,” amesema.

Amesema changamoto kubwa ni kutowafikia Watanzania wote kutokana na upungufu wa rasilimali, lakini amewashauri wananchi kutumia maziwa yaliyosindikwa yanayopatikana kwenye viwanda vya ndani kwa kuwa ni salama zaidi.

“Tuna jumla ya viwanda 187 vinavyosindika maziwa nchini, vikiwemo vidogo, vya kati na vikubwa. Hivyo ni muhimu wananchi waachane na matumizi ya maziwa yasiyo salama yanayouzwa mitaani, hasa yale yanayohifadhiwa kwenye vyombo visivyo rafiki kama vile machupa ya maji,” amesema.

Hillal amesisitiza kuwa matumizi ya maziwa yasiyo salama yanaweza kuhatarisha afya ya mlaji, na hivyo ni muhimu wananchi kuwa makini katika kuchagua maziwa wanayoyatumia kila siku.


WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
BODI YA MAZIWA TANZANIA
TDB
IPANGO WA UNYWAJI
MAZIWA SHULENI
Scan me!

# WANACHAMA TANECU WAJIFUNZA TAFITI ZA UVUVI TAFIRI

Wanachama wa Chama cha Msingi na Ushirika cha Tandahimba and Newala Cooperative Union (TANECU) cha Mkoa wa Mtwara wanaojishughulisha na kilimo cha korosho wamejifunza juu ya tafiti za Uvuvi zinazofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ili kujua jinsi tafiti hizo zinvyosaidia uwekezaji katika sekta ya Uvuvi nchini.

Wananchama hayo walijifunza juu ya Tafiti hizo Agosti 5, 2025 wametembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kwa lengo la kujifunza shughuli mbalimbali za utafiti zinazofanywa  na TAFIRI, wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Nane Nane Mkoani Dodoma.

Akizungumza kwenye Banda la TAFIRI Katibu wa chama cha msingi (TANECU) Bw.Mohamed Kitalya amesema lengo la kufanya ziara yao kujifunza  tafiti  mbalimbali za kisayansi zinavyoweza kuongeza tija katika sekta mbalimbali za uchumi, hasa sekta ya uvuvi.

Kwa upande wake, Afisa Uvuvi Mkuu kutoka TAFIRI Kituo cha Kigoma Bw.Julius Assam,  amewahimiza wanachama wa TANECU kutambua na kutumia fursa zilizopo katika sekta ya uvuvi, hasa kwa vikundi vya wakulima na ushirika.

Bw. Assam alibainisha shughuli za uvuvi, ikiwa ni pamoja na ufugaji wa samaki na usindikaji wa mazao ya uvuvi, zinaweza kuunganishwa na kilimo ili kuongeza kipato cha kaya vijijini.

Pia, Wanachama wa TANECU walijifunza juu ya teknolojia ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba, mfumo wa "Vua Uza na Nunua Samaki Kidijitali (PFZ) sanjari na teknolojia ya kukaushia dagaa kwa mfumo wa solar tent dryer.

Elimu iliyotolewa kwa Wananchama hao ni pamoja na shughuli mbalimbali zinazofanywa na (TAFIRI) hasa katika maeneo ya maji baridi na bahari, mbinu bora za uvuvi endelevu, uhifadhi wa mazingira ya maji, pamoja na mchango wa tafiti katika sekta ya uvuvi nchini Tanzania.



# BODI YA NYAMA YAPONGEZWA NA WANANCHI KATIKA UTOAJI WA VIBALI

Bodi ya Nyama Tanzania yapata pongezi za utoaji wa vibali kwa wafanyabiashara ya nyama ikiwemo maduka ya nyama.
Pongezi hizo zimetolewa na wananchi waliofika katika maonesho ya Nane Nane katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma kuanzia Agosti 1 hadi 10, 2025 na kupata elimu juu ya shughuli zinazofanywa na bodi hiyo na namna bodi inavyosimamia miongozo katika biashara hiyo.

Wageni waliotembelea kwenye banda la bodi ya nyama wamefanikiwa kujua taratibu zinazotakiwa katika ufanyaji wa biashara ya nyama na wengi wao walitaka kufahamu kuhusu uuzaji wa nyama nje ya nchi ambapo wananchi hao walielekezwa taratibu za kufuata ili kuweza kupata kibali cha uuzaji wa nyama nje ya nchi.

Katika maadhimisho hayo Bodi ya Nyama imeshiriki kwa kutoa elimu na kuuza bidhaa kupitia wadau wake akiwemo HUSAM, MIKA MEAT na Kili Agro. Bidhaa zilizouzwa na wadau ni pamoja na vifaa sahihi vinavyotumika kwenye maduka ya nyama na machinjio ikiwemo mashine za kukatia nyama, nondo, visu, mizani na friza. Pia kulikuwa na soseji na nyama ya kuku.
Aidha, wananchi hao wameiomba bodi kuongez aukaguzi wa nyama hasa maeneo ya vijijini kwani kumekuwa na uchinjaji holela na ambao unaweza kuhatarisha afya zao kutokana na mifugo inayochinjwa kutokuwa na sifa zinazotakiwa ikiwemo magonjwa.




JAMHURI YA MUUNGANO WA TAN
BODI YA NYAMA TANZ
EXPORT
RAPH
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BODI YA NYAMA TANZANIA

# TALIRI YAAGIZWA KUIBUA NA KUSAMBAZA TEKNOLOJIA ZA MIFUGO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kuziibua na kuzisambaza teknolojia bora za mifugo ili ziwanufaishe wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Dkt.Samia alitoa agizo hilo Agosti 8, 2028 alipotembelea Banda la TALIRI wakati wa Kilele cha Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo 'Nanenane' yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma yakiwa sambamba na kaulimbiu isemayo 'Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (kulia) akimuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI) Prof. Erick Komba (kushoto) kuhusu kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mbari za Mifugo ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa nchini muda mfupi baada ya kufika kwenye banda hilo Agosti 08, 2025 kwenye Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kuziibua na kuzisambaza teknolojia bora za mifugo ili ziwanufaishe wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Dkt.Samia alitoa agizo hilo Agosti 8, 2028 alipotembelea Banda la TALIRI wakati wa Kilele cha Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo 'Nanenane' yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma yakiwa sambamba na kaulimbiu isemayo 'Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Akiwa katika banda la Taasisi hiyo Mhe.Dkt. Samia alipokea taarifa juu ya teknolojia bora za mifugo zinazozalishwa na TALIRI kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo Prof. Erick Komba.
Katika maonesho hayo yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma TALIRI kupitia teknolojia bora za mifugo zilizozalishwa na taasisi hiyo imefanikiwa kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji na wadau mbalimbali wa mifugo zaidi ya 800 waliotembelea banda hilo.

Teknolojia hizo ni pamoja na malisho na mbegu za malisho, mbari bora za mifugo, vyakula vya mifugo pamoja na kuwaelimisha wafugaji hususani wanaofuga kibiashara juu ya kifaa cha mzani wa kisasa wa kupima uzito wa mnyama na kuhifadhi taarifa mbalimbali juu hali ya mnyama na kuwezesha zoezi la kutoa matibabu kwa mnyama.
Aidha, katika maonesho hayo TALIRI imefanikiwa kupata tuzo ya Mshindi wa kwanza katika kundi la Taasisi za Umma Zinazotoa Mafunzo na Utafiti, tuzo hiyo imekabidhiwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.
TALIRI imemshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia kwa kutembele banda hilo, kupata tuzo ya ushindi wa kwanza kwa taasisi za umma kwenye maonesho hayo.

# MPRU YABAINISHA UMUHIMU WA UHIFADHI WA BAHARI KIUCHUMI

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki kikamilifu katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo (Nane Nane) yaliyofanyika kuanzia Agosti 1–8, 2025 jijini Dodoma. Ushiriki huo uliolenga kuelimisha umma na wadau kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa rasilimali za bahari kwa maendeleo endelevu. Maonesho haya yametoa nafasi kwa MPRU kutangaza shughuli mbalimbali za uhifadhi na ulinzi wa rasilimali hizo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kupitia maonesho haya, MPRU imeeleza juhudi zake katika kulinda na kuendeleza rasilimali muhimu ikiwemo matumbawe, nyasi bahari, mikoko, pamoja na ulinzi wa viumbe vya baharini na ikolojia ya bahari kwa ujumla. Aidha, ilisisitiza mchango wa rasilimali hizo katika kukuza uchumi wa buluu na kutoa fursa za ajira na uwekezaji.

Akizungumza katika banda la MPRU, Afisa Masoko wa MPRU, Bi. Halima Tosiri, amebainisha vivutio mbalimbali vya utalii wa baharini vilivyo chini ya usimamizi wa MPRU, ambavyo vinajulikana kwa fukwe za kuvutia, michezo ya majini, na uwepo wa viumbe wakubwa wa baharini kama vile pomboo, papa potwe, nguva (Dugong) na nyangumi.

"Tunaelekea kwenye msimu wa nyangumi katika Hifadhi ya Bahari ya Maingilio ya Mto Ruvuma–Mnazi Bay. Tutakuwa na Tamasha Kubwa la Nyangumi litakalofanyika Mtwara mjini sambamba na safari maalumu za kuwaona nyangumi katika eneo la Mnazi Bay," amesema Bi. Tosiri.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, Bw. Davis Mpotwa, alisema kuwa MPRU inaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa uhifadhi ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinalindwa na kunufaisha taifa kwa muda mrefu.

"MPRU inatekeleza mradi wa urejeshwaji wa matumbawe nchini kote. Hivi sasa tupo katika hatua ya kutoa elimu kwa jamii za pwani kuhusu umuhimu wa matumbawe ili kushiriki kikamilifu katika kuyahifadhi na kutunza rasilimali za bahari," amesema Bw. Mpotwa.

Kwa ujumla, ushiriki wa MPRU katika maonesho ya Nane Nane 2025 umeendelea kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu nafasi ya uhifadhi wa bahari katika kukuza uchumi wa buluu na kuendeleza sekta ya utalii wa baharini nchini.


WIZAR
HIFADHI ZA
Upandaji


UFUNGUZI WA MAONESHO YA WAKULIMA
NANENANE KITAIFA NA KIMATAIFA 2025
MAADHIMISHO YA SIKU YA
NANENANE 2025


UHURU NA UMOJA


TANZANIA
FISHERIES RESEARCH INSTITUTE










JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
bbt
Building a Better Tomorrow


5H-25038




MAONESHO YA KIMATAIFA YA NANE NANE 2025
KIJIJI CHA PROTINI
Mifugo na Uvuvi ni Utajiri
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI


62.9
MAONESHO YA KIM


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BODI YA NYAMA TANZANI


KAMPUNI YA RANCHI ZA TAIFA LIMITED
KONGWA BEEF


WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
5H-25038

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

MINISTRY OF LIVESTOCK AND FISHERIES

**WASILIANA NASI**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
P.O. BOX 2847 Mtumba, Dodoma Tanzania
Barua pepe: barua@mlf.go.tz
+255 (0)22 2861908
+255 26 2322610
+255 (0)22 2861908